MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KARATASI 102/1

1. SWALI LA LAZIMA
   Anwani ilenge mada – mfano hotuba kuhusu vyanzo na suluhu la mauaji katika ndoa za vijana
2. Utangulizi ubainishe
   Itifaki m.f chifu, naibu wa chifu, vijana.
   Maamkuzi
   Hatibu ajitambulishe na akikosa asadhibiwe.
   Atangulize mada.
3. Mwili
   Mtahiniwa ajadili hoja zinazohusu mada. Kila hoja katika aya yake.
4. Hitimisho
   Mtahiniwa atoe mapendekezo yake na ashukuru hadhira kwa kumsikiliza.
5. Mtahiniwa aweza kuweka alama za mtajo mwanzoni na mwishoni mwa insha. Akiweka mwanzoni kisha akose kuweka mwishoni aadhibiwe kimtindo.
   Vyanzo.
   1. Ukosefu wa ushauri nasaha – vijana kujiingza katika ndoa kabla hawajaelewa yaliyomo.
   2. Vijana kukimbilia maisha – kuoa wangali wadogo.
   3. Matumizi ya dawa za kulevya.
   4. Kupanda kwa gharama ya maisha – vijana wanashindwa kutimiza mahitaji ya kimsingi.
   5. Vijana kutegemea wao kwa kila kitu hivyo basi, wanapokuwa wakubwa wanashidwa kujitegemea.

**SULUHU**

1. Ushauri nasaha kwa vijana kabla na wakiwa kwa ndoa.
2. Wazazi kufunza watoto kujitegemea.
3. Kabla ya kuingia katika ndoa, vijana waweze kujikimu.
4. Vijana wafunzwe kuwa wavumilivu.
5. Talaka

6. Kufufua mila na utamaduni za Kiafrika hasa mivigha ya ndoa.
7. Watoto wapelekwe kanisani wangali wachanga ili wapokee mafunzo ya dini yanayofaa.

**2. SWALI LA PILI**

Faida za pikipiki

1. Zimeibuni nafasi za kazi kwa maelfu ya vijana - huzuia uhalifu.
2. Bei ni nafuu – vjana waweza kujimudu.
3. Huweza kufika katika sehemu yoyote ile hata isiyofikika kwa gari.
4. Gharama ya utunzi na vipuli vyake si ghali.
5. Huokoa wakati kutokana na kasi yake.
6. Zimeharakisha uchukuzi – kubeba vitu vidogo vidogo ambavyo kama gari ingebidi kusubiri hadi kiwango kingezeke.
7. Zimerahisisha usafiri wa watu – mfanyakazi aweza kuitumia kwenda kazini.
8. Usafiri wa harakaka kutokana na kasi, kukwepa msongamano wa magari.
9. Serikali imepata pesa – ushuru, leseni.

HASARA

1. Zimechangia ongezeko la ajali nchini - vifo, ulemavu.
2. Vijana wengi wameacha shule na kuwa waendeshaji.
3. Zatumika kutekeleza uhalifu kwa sababu ya kasi yake na kuweza kuingia vichochoroni.
4. Ongezeko la magonjwa yanayosababishwa na baridi kwa sababu ya upepo.
5. Kuharibu mazingira – kelele, moshi.
6. Zimesababisha msongamano barabarani kwa sababu ya wingi wake.
7. Ongezeko la ufisadi – polisi wanaitisha hongo.
8. Imesababisha uzembe – siku hizi watu hawatembei na mwishowe magonjwa mf kisukari.

TANBIHI

Akijibu upande mmoja faida ama hasara atakuwa amejibu nusu; asipite alama 10/20.
Mtahiniwa atoe msimamo wake na asipoutoa italingana na hoja alizozitoa na ni zipi zinapiku zingine. Lakini atakuwa na udhaifu wa mtindo.
Akitoa zinazotoshana /kulingana atuzwe lakini aadhibiwe kimtindo.

3. SWALI LA TATU

1. mtahiniwa atunge kisa kimoja ambacho kitaonyesha maana (ya juu na ya ndani) ya methali hii.
2. kisa kionyeshe mtu anayeonywa na akakataa kisha akafikiwa na shida ile.
3. Akionyesha upande mmoja wa methali, asipite alama kumi.

4. SWALI LA NNE

1. Mtahiniwa aandike hadithi juu ya mtu aliyeshtakiwa.
2. Kosa analolitenda liwahusishe wanawe na mkewe.
3. Apatikane kuwa mkosa.
4. Hukumu itolewe dhidi ya mshtakiwa na hukumu iwe kali.
5. Asipoanza kwa maneno haya amejitungia swali alama 01-02.
6. Akiyaweka mwisho au katikati atakuwa amejitungia swali apate alama 01-02.
7. Akiacha neno au aongezee maneno atakuwa amepotoka apewe alama 03.

TANBIHI

- Mtahiniwa aweze kutunga kisa ambacho mhusika amefikishwa mahakamani kwa kosa alilotenda na lihusishwe aila yake lakini aombe msamaha kwa kuhukumiwa na kuwaacha kwa mfano ufisadi.
- Mhusika amehukumiwa kifungo aombe msamaha kwa aila yake kwa kuwaaibisha.

## UTANGULIZI

Karatasi hii imedhamiria kutathmini uwezo wa mtahiniwa wa kuwasiliana na msomaji na kuwasilisha ujumbe kimaandishi, akizingatia mada aliyopewa. Mawasiliano haya yatategemea ukwasi wa lugha ya mtahiniwa, kwa mfano, kutunga sentensi sahihi, zenye utiririko mzuri kimawazo, lugha ya kuvutia na yenye mawazo asilia, ubunifu mwingi, na hati nadhifu. Kutegemea maagizo ya swali lenyewe na umahiri wa lugha, ni lazima kutilia mkazo mtindo, mada na uwezo wa mtahiniwa kufuata maagizo vilivyo.

Mtahiniwa lazima aisome insha ili aweze kuikadiria akizingatia viwango mbambali vilivyopendekezwa yaani, A,B,C, na D kutegemea mahali popote pale pafaapo.

**KIWANGO CHA D**

**MAKI 01 – 05**

1. Insha ya aina hii haieleweki kwa vyovyote vile, ama uwezo wa mtahiniwa wa kutumia lugha ni hafifu sana, hivi kwamba mtahini lazima afikirie kile anachojaribu kuandika.
2. Mtahiniwa hana uwezo wa kutumia maneno ya Kiswahili kwa njia inayofaa.
3. Lugha imevurugika, uakifishaji haufai, na insha ina makosa ya kila aina ya kisarufi, kimaendelezo, kimtindo, n.k.
4. kujitungia swali na kulijibu.
5. insha ya urefu war obo ikadiriwe hapa.

**VIWANGO TOFAUTI VYA D**

**D- (KIWANGO CHA CHINI) MAKI 01 – 02**

1. Insha haina mpangilio maalum, na haieleweki kwa vyovyote vile. Kwa mfano,

kunakili swali au kujitungia swali tofauti na kulijibu.
2. Kuandika kwa lugha isiyo Kiswahili.
3. Insha za aina hii zifanyiwe uamuzi na kiongozi wa kikundi
4. Yule anayenakili kichwa kutoka karatasi ya maswali lakini hakushughulikia mada inayokusudiwa atakuwa amejitungia swali.

**D (WASTANI) MAKI 03**

1. Utiririko wa mawazo haupo.
2. Insha haieleweki
3. Hoja hazikuelezwa kikamilifu / mada haikukuzwa vilivyo.
4. Mtahiniwa amepotoka kimaudhui
5. Hakuzingatia urefu.
6. Kuna makosa mengi ya kila aina.

**D+ (KIWANGO CHA JUU) MAKI 04 – 05)**

1. Insha hii ina makosa mengi ya kila aina. Lakini unaweza kutambua kile ambacho mtahiniwa anajaribu kusema.
2. Insha ina lugha dhaifu ya Kiswahili na haina mpangilio.
3. Anawasilisha ujumbe kwa njia isiyoeleweka kikamilifu
4. Hana uhakika wa matumzi ya lugha na hupotoka hapa na pale.
5. Mpangilio wa kazi ni hafifu na mtahiniwa hujirudia rudia
6. Mtahiniwa ana athari za lugha ya kwanza k.m papa, badala ya baba, karamu badala ya kalamu,n.k.

**KIWANGO CHA C**
**MAKI 06 – 10**

Kiwango hiki kina makosa yafuatayo.
1. Mada haikukuzwa na kuendelezwa.
2. Anawasilisha ujumbe kwa njia isiyovutia.
3. Hana ubunifu wa kutosha.
4. Anaakifisha sentensi vibaya.
5. Hana msamiati wa kuvutia wala msamiati mwafaka.
6. Kuna makosa mengi ya sarufi, msamiati na hijai (tahajia)

**VIWANGO TOFAUTI VYA C**

**C- (KIWANGO CHA CHINI) MAKI 06 – 07**

1. Mtahiniwa ana shida ya kuwasilisha mawazo yake.
2. Hana msamiati wa kutosha wala muundo wa sentensi ufaao.
3. Mada haijakuzwa na kuendelezwa kwa njia ifaayo.
4. Ana makosa mengi ya sarufi, tahajia na msamiati.

**C(WASTANI) MAKI 08**

1. Anawasilisha ujumbe lakini kwa njia hafifu.
2. Hana ubunifu wa kutosha na dhana tofauti tofauti hazijitokezi wazi.
3. Uakifishaji wa sentensi zake si mzuri.
4. Amejaribu kushughulikia mada aliyopewa.
5. Ana makosa ya hijai, sarufi na msamiati.

**C+ (KIWANGO CHA JUU) MAKI 09 – 10**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri lakini kwa njia isiyo na mvuto.

2. Dhana tofauti tofauti zimeanza kujitokeza japo kwa njia hafifu.
3. Kuna utiririko wa mawazo japo hana ufundi wa lugha unaofaa.
4. Misemo, methali na tanakali za sauti zimetumiwa kwa njia hafifu.
5. Anashughulikia mada aliyopewa kwa utiririko mzuri.
6. Kuna makosa ya sarufi, msamiati na hijai lakini bado insha inaeleweka.

**KIWANGO CHA B**

**MAKI 11 – 15**

1. Mtahiniwa anaonyesha kuimudu lugha vilivyo.
2. Mtahiniwa anadhihirisha kwamba anaweza kutumia lugha kwa urahisi katika kujieleza.
3. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi vizuri.
4. Mtahiniwa ana uwezo wa kutumia lugha kwa ufasaha mkubwa kama vile kuandika sentensi kwa njia tofauti na zikaleta maana sawa.
5. Mada imekuzwa na kuendelezwa kikamilifu.

**VIWANGO TOFAUTI VYA B**

**B- (KIWANGO CHA CHINI) MAKI 11 – 12**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe wake kwa kuonyesha hoja tofauti tofauti akizingatia mada.
2. Ana utiririko mzuri wa mawazo.
3. Ana uwezo wa kutumia mitindo tofauti tofauti ya sentensi.
4. Makosa ni ya hapa na pale.

**B(WASTANI ) MAKI 13**

1. Mtahiniwa anadhihirisha hali ya kuimudu lugha.
2. Anawasilisha ujumbe wake waziwazi kwa mawazo yanayodhihirka akizingatia mada.
3. Matumizi ya lugha ya mnato yamejitokeza.
4. Anatumia mifano michache ya msamiati teule /mwafaka.
5. Matumizi ya tamathali za usemi yanaanza kudhihirika.
6. Makosa machache ya hapa na pale.

**B+ (KIWANGO CHA JUU) MAKI 14 – 15**

1. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika – yanajitokeza waziwazi
2. Anawasilisha ujumbe wake kwa njia inayovutia huku akizingatia mada.
3. Uteuzi wake wa msamiati ni mzuri.
4. Sarufi yake ni nzuri vilevile uakifishaji wake.
5. Makosa yanaweza kutokea hapa na pale.

**KIWANGO CHA A**

**MAKI 16 – 20**

1. Mtahiniwa anadhihirisha ujuzi wa lugha yenye mnato.
Ana ubunifu wa mawazo yanayodhihirika na kutiririka .
2. Ana uwezo wa kutumia tamathali za usemi ili kutoa husia zake kwa njia bora.
3. Umbuji wake unadhirisha ukakamavu wake kimawazo na mpangilio mzuri na hali ya kumvutia msomaji wake.

4. Kazi ya mtahiniwa ni nadhifu na hati ni nzuri .
5. Insha hii imezingatia urefu unaotakikana

**VIWANGO TOFAUTI VYA**

**A- (KIWANGO CHA CHINI) MAKI 16 - 17**

1. Mtahiniwa anadhihirisha ukomavu wa lugha.
2. Ana utiririko mzuri wa mawazo kulingana na mada.
3. Anapamba lugha kwa kutumia tamathali za usemi.
4. Anazingatia matumizi ya msamiati na sarufi
5. Uakifishaji wake ni mzuri zaidi.
6. Makosa machache yasiyokusudiwa.

**A (WASTANI) MAKI 18**

1. Mawazo yanadhihirika zaidi na anashughulikia mada aliyopewa.
2. Anatumia lugha ya mnato.
3. Anatumia msamiati wa hali ya juu na unaovutia.
4. Sarufi yake ni nzuri zaidi.
5. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi kiufundi.
6. Anajieleza kikamilifu na makosa ni nadra kupatikana.

**A+ (KIWANGO CHA JUU ) MAKI 19 – 20**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe kulingana na mada.
2. Anadhihirisha mawazo yake vizuri zaidi.
3. Anatoa hoja zilizokomaa.
4. Msamiati wake ni wa hali ya juu.
5. Jumla ya makosa yote yaisizidi matano.

| KIWANGO | NGAZI | MAKI |
|---|---|---|
| A | A+<br>A<br>A- | 19-20<br>18<br>16-17 |
| B | B+<br>B<br>B- | 14-15<br>13<br>11-12 |
| C | C+<br>C<br>C- | 9-10<br>8<br>6-7 |
| D | D+<br>D<br>D- | 4-5<br>3<br>1-2 |

**JINSI YA KUTUZA INSHA MBALIMBALI.**

1. Mtahiniwa asipozingatia sura ya insha aondolewe maki nne(4) baada ya kutuzwa (4 sura)
2. Insha isiyotoshele idadi ya maneno itaondelewa maki mbili(2) baada ya kutuzwa.(2u)

**SARUFI**

Sahihisha kwa makini sana ukionyesha makosa yote yanayotokea.
Makosa ya sarufi huwa katika:-

1. Kuakifisha vibaya.Kwa mfano, vikomo, vituo, alama ya kuulizia , n.k

2. Kutumia herufi ndogo au kubwa mahali si pake.
3. Matumizi mabaya ya ngeli na viambishi, nyakati, vihusiano, muundo mbaya wa sentensi
na mnyambuliko wa vitenzi na majina.
4. Kuacha au kuongeza neno katika sentensi, kwa mfano, “kwa kwa”
5. matumizi ya herufi kubwa:
a) Mwanzo wa sentensi
b) Majina ya pekeei)
I)Majina ya mahali, miji,nchi
ii) Siku za juma,miezi, n.k
iii) Mashirika, masomo,vitabu,n.k
iv) Makabila, lugha, n.k
v) Jina la Mungu
vi) Majina ya kutambulisha k.m majina ya mbwa k.v Tom, Jim, Peter

**MAKOSA YA HIJAI / TAHAJIA.**

Haya ni makosa ya maendelezo. Sahihisha huku ukiyaonyesha yanapotokea.
Makosa ya tahajia huwa katika:-
1. Kutenganisha neno kama vile ‘ aliye kuwa’
2. Kuunganisha neno kama vile ‘kwasababu’
3. Kukata silabi vibaya kama vile ‘ngan-o’
4. Kuandika herufi isiyofaa katika neno kama ‘ mahari’ badala ya ‘mahali’
5. Kuacha herufi katika neno kama vile ‘aliekuja’ badala ya aliyekuja.
6. Kuongeza herufi isiyofaa katika neno kama vile ‘piya’ badala ya pia’
7. Kuacha alama inayotarajiwa kuwepo katika herufi k.m j,i
8. Kutoandika kistari cha kuunganisha neno ufikiapo pambizo au mwisho ‘ au kukiandika
mahali si pake.
9. Kuacha ritifaa au kuiweka pasipofaa. K.m Ngombe,ngom’be, n’gombe.
10. Kuandika maneno kwa kifupi .Kwa mfano,k.m n.k,v.v,k.v

**MTINDO**

**Mambo yanayochunguzwa:**

1. Mpangilio wa kazi katika aya.
2. Utiririko wa mawazo
3. Hati nzuri inayosomeka kwa urahisi.
4. Namna anavyotumia tamathali za usemi k.m methali, misemo, jazanda n.k
5. Kuandika herufi vizuri k.m Jj, pp, Uv,n.k
6. Sura ya insha
7. Kuorodhesha.

**MSAMIATI**

Jumla ya maneno yaliyotumiwa kuafikiana na mada au kichwa kilichopendekezwa.

**MAUDHUI NA MSAMIATI.**

Baada ya kusoma mtungo utafikiria maudhui na msamiati uliomo kwa jumla.

**ALAMA ZA KUSAHIHISHA**

= Hupigwa chini ya sehemu ambayo kosa la sarufi limetokeza kwa mara ya kwanza tu.
Hupigwa chini ya sehemu au neno ambako kosa la hijai limetokeza kwa mara ya kwanza tu.

Hutumiwa kuonyesha kuachwa kwa neno.
_ Hutumiwa kuonyesha msamiati bora. Alama hii hutiwa juu ya neno lenyewe.
X Hutumiwa kuonyesha msamiati usiofaa .Alama hii hutiwa juu ya neon lenyewe
Maelezo mafupi kuhusu tuzo la mtahini yanahitajika
Kila ukurasa uwe na alama ya _ chini katikati kuonyesha kuwa mtahini ameupitia ukurasa huo.

**MANENO**

Maneno 8 - Ukurasa 1 ¾
Maneno 7 - Ukurasa 2
Maneno 6 - Ukurasa 2 ¼
Maneno 5 - Ukurasa 2 ¾
Maneno 4 - Ukurasa 3 ¾
Maneno 3 - Ukurasa 4 ½

**MANENO**

101 – 174 - Nusu
175 - 274 - Nusu
275 – 374 - Robo tatu
375 – 400 -Kamili